

Mwongozo wa swali la kwanza

Kiswahili (102)

Swali la kwanza

Tahariri kwa gazeti la Alwodo

a) Sura

- Iwe na kichwa cha gazeti
- Iwe na terehe
- I we na utangulizi.
- I we na mwili/maelezo kiaya
- Inaweza kutoa maoni au msimamo wa mhariri

b) Maudhui

- Umaskini unafanya wengi kukosa mahitaji ya kimsingi
- Uyatima – Kufiwa na mzazi na kuwachwa bila wa kutegemewa.
- Mazingira magumu shuleni kama vile adhabu kali ambayo husababisha wao kuwacha masomokujunga na ajira.
- Shirikizo la rika kuwashawishi wajunge na ajira za mapema.
- Matumizi ya dawa za kulevyaa ambazo huchochea mahitaji ya kununua dawa hizi na kuwafanya wanafunzi watafute ajira za mapema.
- Kushawishiwa na waajiri kwa sababu ajira ya watoto ni nafuu ikilinganishwa nay a watu wazima.
- Ufisadi – waajiri wa watoto kutochukuliwa hatua na waliopewa jukumu.
- Changamoto za shule kuwa mbali na kuwavunja watoto moyo wa kuendelea na masomo.
- Wazazi wenye uwezo mdogo wa kifedha hutumia wato wao kufanya kazi.
- Watoto kutolalamika kutookana na unyonge wao
- Hufanya waajiri kuwapendelea
- Kaduria hoja za mtahiniwa.

SWALI LA PILI

- Hii ni insha ya mjadala.
- Mtahiniwa ajadili pande zote mbili kasha aonyeshe msimamo wake.
- Mtahiniwa akiiegemea upande mmoja allama zisizidi kumi.
- Atakayekosa kutoa msimamo alama za sura ziondolewe(-45)
-

Uzuri/Manufaa

- a) Tarakilishi imerahisisha utafti mionganii mwa wanafunzi.
- b) Baadhi zinaweza kuhifadhi umeme.
- c) Baadhi zinaweza kutumiwa mahali popote
- d) Zinapunguza gharama ya kununua vitabu vya kiada.
- e) Wafunzi wanaweza kutumia wakati wowote bilauwepo wa mwalimu.
- f) Huhifadhi ujumbe mpana.
- g) Inawapa wanafunzi ujuzi wa kutumia teknologia kwa mawanda.

Hasara

- a) Ina gharama ya juu kununua na kutunza .
- b) Inapotosha kimaadili kwani baadhi watatazama mambo mengine ya kupotosha.
- c) Baadhi ya wafunzi na wqalimu hawajui kutumia tarakilishi.
- d) Inahitaji nguvu za umeme na kuna baadhi ya sehemu ambazo hazina nuvu za umeme

- e) Inadhuni kiafya kwa kuathiri macho na hata mgongo kukaa kwa muda mrefu
- f) Ni vigumu kwa wale walio na kasoro ya kuona.

TANBIHI

Atakayezingatia hasara /uzuri atakuwa amepungukiwa kimaudhui. Asipite kiwango cha C + (09-10)

Swali la tatu (mwongozo)

Hii ni insha ya methali ambapo kisa lazima kithibitishe ukweli wa methali

Maana

Anayecheka wenginewalio na tatizo lolote utafika wakati wake na atapatwa na tatizo sawia.

Matumizi

- a) Hutumika kutahadharisha wale wanaocheka wenzao wanapokuwa na janga, kwani wakati wao utafika.
- b) Kisa kionyeshe hali ambapo mtu alisherehekeea wakati wenzake walikuwa na shida nae kapatwa na shida hio hio.

Tathmini haya;

Kisa kinawenza kudhihirisha hali zifuatazo:

- i. Mtu asherehekeea mwenzake akifiwa na baadaye pia afiwe.
- ii. Mwanafunzi amcheke.
- iii. Tajiri amcheke maskini kisha mali yakeipotee baadaye awe maskini.
- iv. Mtu mzima amudhihaki mgonjwa naye apatwe na ugonjwa baadaye.

Tanbihi

1. Lazima kisa kitoe pande mbili za methali.
 - a) Kucheka kilema
 - b) Kilema kumpata

Atakayezingatia upande mmoja tu amepungukiwa maudhui asipite lama (C wastani)

2. Atakayetunga kisa lakini kisidhihirishe ukweli wa methali anupunguvu wa kimtindo aadhibiwe kimutindo
3. Atakayekosa kutunga kisa yaani atumie mifano tu achukuliwe kama aliyepotokwa kimaudhui na awewe katika kiwa cha D 03/20.
4. Si lazima mtahiniwa aeleze maana ya methali.

Swali la nne

- i. Hii ni insha ya mdokezo ambapo mtahiniwa lazima aanze kwa mdokezo aliopewa.
- ii. Kisa cha mtahiniwa sharti kikamilike kwa huu mdokezo.

Jibu

- a) Yawezekana uwe ni mkasa wa moto shulen.
- b) Au uvamizi uliofanyika.
- c) Au wizi ulifanyika wa mtihani au chochote kile kisha anajutia kwa sababu alifahamu jambo hilo.
- d) Kutekwa nyara (mionganoni mwa mambo mengine)

Tanbihi

1. Insha zote lazima zitimize urefu uliokusudiwa. Upungufu wowote utashughulikiwa kulingana na mwongozo wa kudumu.
2. Insha zote (2, 3 na 4) lazima ziwe na vichwa. Mtahiniwa akiacha achukuliwe kuwa amepungukiwa kimtindo.
3. Mtahiniwa lazima asome kwa makini mtungo wa mtahiniwa akizingatia mada na matumizi ya miongozo miwili yaani, wa maswali na viwango ili kuweka insha ya mwanafunzi katika kiwango chake.